



السواحيلية  
SWAHILI

إرشادات عامة  
للقوى العاملة غير العمالية  
للعمل في سلطنة عُمان

MWONGOZO KWA WAAJIRIMA  
WA KIGENI NGHINI OMAN

# MWONGOZO KWA WAAJIRIWA WA KIGENI NCHINI OMAN

**Wapendwa Waajiriwa wa Kigeni,**

**Tungependa kuwajulisha mambo  
muhimu yanayohusu mahusiano yenu  
na waajiriwa wenu kama ituatavyo:**

- Unapowasili nchini Oman, unatakiwa kutoa taurifa Ofisi ya Ubalazi wa nchi yako. Iwapo hufahamu namba yao ya simu, unaweza kupiga Nambari **(1318)** kwa maelezo.
- Unapowasili nchini Oman kwa kufanya kazi, na unashindwa kufika katika anwani husika, unaweza kupiga nambari maalum **(80077000)** au fika Wizara ya Kazi.
- Iwapo taratibu zinazohusiana na kitambulisho chako cha kazi au ukaazi hazijakamilika katika kipindi cha mwezi mmoja tangu kuwasili, basi unapaswa utoe taurifa kwa mamlaka husika, Wizara ya Kazi.
- Kitambulisho cha kazi (au kadi ya ukaazi) ni hati rasmi na muhimu; tafadhali zitunze vizuri.
- Usisubiri kumalizika muda wa pasipoti yako; tafadhali omba nyingine kabla haijamalizika muda.
- Unaweza kuomba kupatiwa nakala ya mkataba wa kazi ambao utakuwa nao ili kuelewa haki na wajibu wako.



- Iwapo huridhiki na kazi uifanyayo, usiamue kuacha kienyeji kwani unaweza kukabiliana na matatizo ya kisheria.
- Wasiliana na Ubalozi wako mara unaposimamishwa na polisi. Unapokuwa na tatizo lolote katika kituo cha polisi, utatakiwa kutumia simu mara moja tu. Tafadhali wasiliana na Ubalozi wako na sio rafiki.
- Ni haki yako kupatiwa bima na mdhamini/mwajiri wako dhidi ya ajali kazini na maumivu.
- Mshahara wako wa mwezi utakapocheleweshwa una haki ya kuudai toka kwa mwajiri wako. Iwapo hakuna majibu, unaweza kuarifu mamlaka husika, Wizara ya Kazi.
- Iwapo utalazimika kufanya kazi masaa ya ziada, mwajiri atapaswa kukulipa kwa mujibu wa kanuni za Sheria ya kazi ya Oman Namb. **35/2003**.
- Iwapo kutakuwa na mgogoro au kutoelewana na mwajiri wako au mwakilishi wake na mkashindwa kufikia suluhu, unawajibwa kutoa taurifa mamlaka husika, Wizara ya Kazi.
- Iwapo ajira yako itasitishwa bila sababu za msingi, unawajibwa kutoa taurifa Wizara ya Kazi kuzuia kusitishwa huko ndani ya siku 15 tokea kusitishwa kwa ajira.
- Usiache kazi kwa mwajiri wako na usifanye kazi kwa mwajiri mwingine ambaye hujaruhusiwa. Kufanya hivyo ni kosa na kutapelekea kuchukuliwa hatua za kisheria, ikiwemo kifungo na faini dhidi yako.

- Kumbuka kwamba mwajiriwa anayefanya kazi Oman bila kibali cha kufanya kazi kutoka Wizara ya Kazi au cha kufanya kazi kwa mwajiri, anaweza kuadhibiwa kifungo cha mwezi mmoja jela na faini isiyozidi **Riali 100** za Oman, au adhabu zote pamoja na kufutwa kwa kibali (ikiwa kipo).
- Tafadhali elewa kwamba mwajiriwa yeyote atakayekamatwa akifanya kazi isiyo halali, ataingizwa kwenye orodha ya wenye dosari (**black list**) na haturuhusiwa tena kuingia Oman.
- Mwajiriwa anaweza kupoteza haki zake anazodai mara utakapomalizika muda wake mwaka mmoja tangu kumalizika kwa mkataba wa ajira yake.
- Tafadhali toa ushirikiano kwa maafisa wa Serikali. Ni kosa kwa mtu yeyote kuwazuia maafisa watumishi wa Serikali kufanya kazi zao; kosa hilo linapelekea adhabu ya faini ya **Rial 100** na kifungo cha mwezi mmoja jela, au zote mbili pamoja. Adhabu hizo zinaweza kuwa maradufu iwapo kosa litarudiwa.
- Kufuata taratibu za kiafya na usalama kazini zitakulinda na kukuhifadhi dhidi ya ajali kazini.
- Mgomo kazini unaelezwa chini ya taratibu halali zilizotolewa na Wizara ya Kazi. Tafadhali elewa taratibu hizo kabla ya mgomo. Kugoma hakuruhusiwi katika taasisi zinazotoa huduma muhimu kwa jamii.

- Tafadhali heshimu dini ya Kiislam na zingatia kanuni, taratibu na maadili yaliyopo Oman. Usijilingize au kujihusisha na vitendo vyovyote vyenye kuhatarisha usalama wa taifa.
- Mwajiri anapaswa kulipa mshahara bila kukosa.
- Si ruhusa kufanya kazi kwa mtu mwingine hadi itakapopatikana barua ya ruhusa (**release letter**) na kukamilika kwa taratibu vingine za kisheria.

**Tunawatakia kheri na mafanikio.**

[www.mol.gov.om](http://www.mol.gov.om)





لمزيد من المعلومات يرجى زيارة  
الموقع الإلكتروني لوزارة العمل



استخدم رمز الاستجابة  
السريع لتحميل  
تطبيق معاك

Download on the  
App Store

GET IT ON  
Google Play

بكل خطوة  
At Every Step

معاك  
M A ' A K

سَلْطَنَةُ عُضْمَانِ  
وَزَارَةُ الْعَمَلِ

وزارة العمل-سلطنة عُمان  
مرتفعات المطار-مسقط

مركز الاتصال  
800 77 000

www.mol.gov.om

f @ /labour\_oman